


# K.O.K.W.A

Na: Richard MWAMBE

©Jamvi la Simulizi 2025

## SEHEMU YA 5

***Ilipoishia...***

**"Sasa kazi inaanza!" akajisemea na kuchukua bastola kutoka kwenye lile gari, akaikagua na kuhakikisha ipo sawa. Akafyatua kitasa cha mlango, akateremka na kulirudia lango. Sasa kamanda Amata alikuwa akiongozwa na hasira zaidi kuliko utashi. Akatoka nje ya uzio na kuvuta hatua kuelekea Ofisi ndogo za Bunge. Lengo lilikuwa ni kumtaka mmiliki wa hilo gari na nani alikuwa akiendesha. Aliamini kuwa hao wangeweza kumfanya ampate Braison Sambala. Na kupitia wao angeweza kuanza kuingia ndani ya hujuma na kugundua tatizo. *Je wanahusika na upotevu wa Kokwa au kuna jingine?* Akajiuliza.**

✠ ✠ ✠

***Endelea...***

Mchana wa siku hiyo, wafanyakazi wachache sana walikuwa katika ofisi zao. Wengi walikuwa wametoka kwa Chakula cha Mchana na wengine walienda msikitini. Amata alipanda ngazi kufika ghorofa ya kwanza ambapo alipokelewa na mwanadada mrembo aliyekuwa nyuma ya dawati la mapokezi.

"Karibu sana kaka nikusaidie," akamwambia Amata.

“Asante kwa wema wako… unaonekana u mwema sana… samahani naweza kumpata mmiliki wa gari hilo hapo chini?” akauliza.

“Lipi?” yule mwanamke akauliza.

“Hilo Mazda!”

“Enhe walitakia nini mi’ ndiye mmiliki…” yule mwanadada akaeleza bila kujua lengo la muulizaji. Kwa upande wa Amata.

“Nashukuru kukufahamu, nahitaji tuongee biashara, mimi mgonjwa sana wa aina hii ya magari…” Amata akasema, “Lakini sijakujua hata unaitwa nani… mimi naitwa Jaffar,” akasema.

“Naitwa Nuru Sembaga!”

“Nuru… unasemaje?” Amata akauliza. Nuru alipogongana macho na mwanaume huyo aliinama chini.

“Siuzi bwana! Gari lenyewe bovu si umeona limebonyea bonet, sijui ilikuwaje… nimeogopa hata kuuliza,” Nuru alieleza. Na kweli hata Amata aliona lile bonyeo na kujihakikishia kuwa gari analolitafuta hakika ni hilo.

“Mwambie Shemeji kuna mteja analihitaji, kama yupo tayari kuliuza basi afanye hivyo,” Amata akamwambia na kutoa wallet yake. Akachomoa kadi yake ya mawasiliano na kumpatia Nuru, “Hii hapa namba yangu na email na kila kitu. Mwambie asevu namba yangu ili akinihitaji kwa biashara basi anipigie, au nipe ya kwake… lipi jema?” Aamata akamtega Nuru. Masikini Nuru bila kujua akaingia mtegoni. Yeye kwake aliona usalama ni kutotoa namba ila kuchukua ile kadikazi ya Amata. Laity angejua kuwa aliye mbele yake ni jasusi mbobevu na hatari katika Bara la Afrika na kwingineko asingethubutu hata kukubaliana biashara naye. “Asante Bi. Nuru, nitafurahi kukuona tena…” Amata akaaga na kuondoka. Wakati akiteremka ngazi akachukua kutoka mfuko

mwake kitu kidogo kama kifungo. Akabandua upande mmoja nacho kikabaki na unato. Amata akapita jirani na lile gari na kukibandika chini ya kioo cha pembeni yaani *side mirror*. Akaondoka zake. Moyoni mwake akijua sasa ni mambo mawili; mosi lukifuatilia lile gari likitoka pale baada ya kupachika kidubwasha kinachoweza kuonesha uelekeo wa gari lile, pili kusubiri, kama yule bwana atapokea ile kadi kazi na kuingiza zile namba basi tayari katika simu hii maalumu ya Amata angeweza kuzinasa simu zake zote na mawasiliano mengine.

✠ ✠ ✠

Katika chumba maalum, Madam S alikuwa amelala kimya. Pemebeni yake alikuwapo Gina katika mavazi ya kiuguzi na Jasmini katika mavazi ya kitabibu. Zaidi ya wao kubadilishana mawazo kwa sauti za chini, basin i sauti za mashine tu ndizo zilizosikika. Mlango ulikuwa umefungwa kwa ndani, hakuruhusiwa mtu yeyote kutoka nje kuingia ndani ya chumba kile. Saa ishirini na nne zilikwishapita tangu ajali ile itokee na Madam S hakuonesha kabisa dalili ya kuamka.

Mchakacho wa hatua za binadamu ulisikika kwa mbali kwenye korido za jengo lile. Mtu huyo alikuwa akikikaribisa chumba hicho. Gina na Jasmini walishausikia mjongeo huo uliokuwa kwa kiwango ambacho sikio la mwanadamu la kawaida lisingeweza kusikia. Ukimya ukatawala, nasekunde kumi baadae mlango ukagongwa. Mtindo uliotumika kugonga mlango huo wote wawili waliujua. Gina alikuwa wakanza kuinuka huku mkono wenye bastola iliyofungwa kiwambo cha sauti ukiwa nyuma na mwingine ukisungusha funguo ya ule mlango.

Hawakukosea, Kamanda Amata alikuwa mbele ya mlango ule.

"Karibu Kamanda!" Gina akamkaribisha huku akiufunga ule mlango kama mwanzo mara baada ya kijana huyo kuingia ndani. Jasmine alishusha pumzi ndefu na kuirudisha bastola yake pahala pake.

"Asante, mbona mmekaa kisharishari hivi?" akawauliza.

"Lazima tukae kisharishari, hali si nzuri kabisa kamanda," Jasmini akawa wa kwanza kujibu.

"Msiwe na wasiwasi kila kitu kipo under control, anaendeleaje HOT?" akawafariji na kuwauliza.

"Kama unavyoona, saa la ishirini na mbili sasa bado hajaamka… lakini kila kitu kipo sawa kama unavyoona," Jasmini akamwambia Amata.

"Na huko nje vipi? Maana kwa kuchelewa huku ina maana kuna kazi ulikuwa unafanya," Gina akazungumza kwa upole. Amata akageuka kumtazama msichana huyo.

"Eh mwenzangu umekuwa muuguzi siku hizi?" akamtania, "Huko nje nimeshaweka mambo sawa, na muda si mrefu nitajua hii mbinu imepangwa na nani na kwa kusudi lipi, yaani hapa nasubiri jibu tu…" Amata akaeleza. endapo ungekutana na kijana huyu barabarani au kwenye harakati nyingine usingeweza kudhani kama ni mtu hatari kiasi hichi kinachoelezwa vitabuni. Ni shababi, mpole wa tabia, mwenye utani mwingi, lakini daima huwa akiwaacha na hali mbaya wanawake wenye uchu.

"Hapo sawa," Gina akajibu.

"Nimekuja kumuona Boss halafu nikaendelee na kazi yangu, ninyi mubaki hapahapa, nitawaruhusu kutoka tu nikiwa na jibu la uhakika kuhusu jambo hili, maana nahisi kuna kazi kubwa huko

mbele inatukabili," akawaambia na wote wawili wakajibu kwa kutikisa vichwa. "Kwahiyo tahadhari yetu iendelee hivihivi, hapa mlipo ni sehemu salama, hakuna mjinga yeyote anayepajua na atakayefika… najua kama walitaka kumuua basi sasa wanahaha kutafuta wapi alipo, na hata wakijua, hapa hawawezi kufika …" Amata akawaambia. Madam S, mara baada ya kufikishwa Muhimbili, hakukaa hata saa tatu pale, Amata alimwagiza Gina kuwa mwanamama huyo ahamishiwe Hospitali ya Mzena lakini Jasmini alipojua hali ya Madam S albadili mawazo na kumpeleka Jabal Hira Clinic na kumficha huko. Jabal Hira Clinic ilikuwa chini ya Daktari huyo kutoka TSA, na waliitumia mara nyingi kwa matibabu yao ya siri.

Wakiwa katika mazungumzo hayo, mara wakamsikia Madam S akikohoa. Wote wakageuka upande ule wakati Jasmini akizunguka kitanda kwenda kwenye mitambo yake. "Ameamka sasa… tena akiwa na akili zake," akawaambia.

"Aliyewaambia mi nimezimia nani? Nilikuwa nimepumzika tu…" Madam S akasema kwa sauti isyo ya mgonjwa. "Mi nilikuwa nimepumzika tu, nikiwasikiliza kwa kila mnaloliongea tangu jana mpaka sasa," akaongeza kusema. "Amata hongera kwa ulipofikia najus si pabaya sana… lakini tutaongea vizuri tuna mambo mengi na muhimu ya kufanya. Msione nilikuwa kimya kitandani nilikuwa napanga na kupangua kila jambo," akawaeleza huku akijivuta kuketi pale kitandani.

"Ila Madam, kwanini kutuweka roho juu watoto wako? Yaani umefumba macho saa ishirini nan ne bila kujitikisa kweli!" Gina akalalama.

"Eee, hiyo ndiyo kazi ya mpelelezi bingwa hasa anapotaka kupata habari za adui yake, anajinasisha kwenye mtengo halafu

wakimpiga kidogo anajifanya amezimia hata kama ni saa sabini na mbili unalala kimya unasikiliza kila kitu wanachoongea. Kama hujapata hayo mafunzo basi ngoja tumalize hili sakata nikupeleke kwa miezi mitatu Israel. Kule utajifunza kupunguza mapigo ya moyo wako au kuyaongeza kasi, utajifunza kuzimia nusu na kubaki hai nusu, utajifunza mpaka kufa na kufufuka… wale watu achana nao," akasema huku akiinuka na kusimama wima. Madam S aliinuka kutoka pale kitandani na kuuelekea mlango wa maliwato. Dakika tano zilimtosha na kutoka akiwa mpya kabisa na mwenye nguvu.

"Ulimpa Recho taarifa?" akamuuliza Gina.

"Ndiyo!" Gina akajibu.

"Sasa tuelekee Shamba, tuna mambo ya kuweka sawa, Amata umewasiliana na vijana wako?"

"Ndiyo Madam, Chiba na Scoba wote wapo tayari wanasubiri amri tu…" Amata akaeleza.

Mazungumzo ya wanne hao yalichukua takribani dakika kumi hivi, na kishapo wote wakaelekea kwenye gari la Gina. "Tuna kazi kubwa, kila mmoja nitampa kipande chake!" Madam S akawaambia.

"Ila we inabidi upumzike sasa…" Amata akamwambia.

"Nipumzike kwa lipi? Nina maumivu tu kidogo kwenye mbavu… lakini siyo ya kunifanay nishindwe kazi," Madam S akaeleza wakati tayari Gina akiwa barabarani kuelekea Kigamboni yaliko makao makuu ya TSA. Shamba, jumba lisiloishi mtu, ni TSA tu ambao hukutana kwa kazi zao. Majirani wa eneo hilo walizoea kuliita jumba hilo kuwa ni 'Ghost House' maana ni mara chache waliona mtu akiingia lakini zaidi huona taa zikiwaka na kujizima zenyewe ifikapo jioni na asubuhi mtawalia.

Wakati safari nzima ikiendelea Madam S alikuwa kimya kabisa, alionekana kuwa na mawazo mengi, lakini hakuna aliyejua nini hasa alikuwa akikiwaza. Mwendo wa saa moja na dakika kama kumi hivi, waliwasili katika jumba hilo. Kwa kupitia lango la nyuma waliingia moja kwa moja mpaka kwenye maegesho yaliyojengwa ndani ya jengo hilo. Lango kuu likajifunga nyuma yao.

"Nataka uchunguzi ufanyike kuhusiana na sakata zima la kupotea Kokwa pale Makumbusho ya Taifa," akamwambia Amata wakati wakipiga hatua kuingie kwenye sebule kubwa. Gina na Jasmini bado walibaki nyuma.

"Una lolote katika hilo?" Amata akamwamuuliza.

"Namba Moja keshatoa maelekezo… we cha kufanya sasa ni kujua ile Kokwa imetowekaje pale Makumbusho," Madam S akasema huku akiingia ofisini kwake.

"Na ajali iliyokupata unafikiri inahusiana na hili suala?" Amata akarusha swali jingine.

"Sijui, achana nalo!"

"Hapana, siwezi kuachana nalo maana nimeshaanza kuona jambo zito nyuma yake," Amata akajibu. Madam S akabaki kimya akimkazia sura mwanaume huyo.

"Jambo gani?"

"Labda uniambie ilikuwaje, ulijisahau ukaingia barabarani kwa mawazo au ulisukumwa na mtu?" Amata akahoji.

"Mh! Nahisi nilisukumwa na mtu, si unajua kwenye zile korido wa tu ni wengi…" Madam S akajibu.

"Haikuwa ajali ya bahati mbaya, ilikusudiwa…" Amata akaeleza. Mwanamama yule akashusha pumzi na kujiegemeza kitini.

“Umeshajua yote hayo?” akauliza.

“Na ndiyo maana sikuja kukuona kwanza… na muda si mrefu nitampata mhusika aliyepanga misheni hiyo. Kwa vyovyote kuna jambo ndani yake, ila nataka kujua kama likahusiana na Kokwa au ni uadui tu wa kawaida…” Amata akaeleza. “Umeshawahi kumsikia Braison Sambala?”

“Ndiyo! Ni jambazi hilo linalowatoa jasho polisi,” Madam akajibu.

“Umeshawahi kumuona?”

“Hapana!”

“Basi, Braison Sambala ndiye aliyeku-push pale kwenye korido nawe ukaangukia barabarani,” Amata akamwambia.

“Unasema!”

“Ee ndiyo hivyo, na nimeifuatilia ile gari iliyokugonga…”

“Enhe…”

“Mara baada ya kukugonga ilienda kuegeshwa katika ofisi ndogo za Bunge,” Amata akaeleza.

“Weeee… unataka kuniambia nini?” Madama akauliza kwa hamaki.

“Kikulacho ki nguoni mwako,” Mata akajibu.

## SURA YA 3

**DUMILA – MOROGORO**

Katika Kijiji cha Kibaoni, pembezoni tu mwa Mto Mkondoa, ndani ya jumba kubwa lenye ghorofa mbili lililojitenga na makazi ya watu, kulikuwa na kikao cha watu watatu. Wawili Waafrika na mmoja Mzungu mwenye nywele nyeupe pe. Mzungu huyu aliyejulikana kama Mwekezaji alijenga jumba hilo miaka kadhaa nyuma akiendesha shughuli za kilimo cha miwa na vitu vingine. Mwendo wa kilomita moja kutoka kwenye lile jumba kando kando ya mto huohuo, alijenga kiwanda kikubwa cha kuchakata miwa hiyo na kuwa sukari safi ya daraja la juu na kuuza nje ya nchi, na ile ya daraja la chini aliiuza katika soko la ndani. Mwekezaji huyo aliyetoa ajira zaidi ya mia moja kwa wakazi wa Dumila hasa kijiji cha Kibaoni alikuwa raia kutoka Russia kawenye Kisiwa cha Novaya Zemlya. Katika Kisiwa hiki kuna maeneo mawili makubwa ambayo watu wachache sana huishi na ni kwa sababu maalum. Kisiwa hiki kilundwa na visiwa viwili vikuu: Kisiwa cha Severny upande wa Kaskazini na Yuzhny upande wa Kusini. Kisiwa hiki kilikuwa ni sehemu ya Urusi

karibu kabisa na ukanda wa Aktiki. Hakuna ndege ya umma inayofika huko zaidi ni za kijeshi tu. Nazo hutu kwenye uwanja wa jeshi wa Rogachevo katika upande wa Yuhzny.

Makundi matatu ambayo hufika huko ni wanajeshi, wanasayansi na ujumbe wa serikali ya Urusi na kama kuna mgeni basi ni lazima apate kibali maalum cha kijeshi. Kisiwa hiki kilikuwa na baridi kali sana, barafu ya muda wote na makazi ya watu wachache mno.

Kisiwa hiki kilikuwa eneo lililojulikana zaidi kwa majaribio ya silaha za nyuklia na umoja wa Kisovieti nyakati hizo za 1955 – 1990. Hapa ndipo lilipofanyiwa majaribio bomu kubwa sana kuwahi kulipuliwa, Tsar Bomba. Na sasa limebaki kuwa eneo la kijeshi linalofikiwa kwa kibali maalum tu. Huyu mwekezaji alijulikana kwa jina moja tu Mikhail.

“Mlitakiwa kuhakikisha anakufa kabisa,” Mikhail aliwaambia vijana aliyokuwa nao hapo ndani.

“Ni kweli, kuna mistake pale imetokea lakini hata hivyo tutampata tu…” kijana mmoja akajibu.

“Swala siyo kumpata, tumepewa tahadhari kuwa, huyu mama akifikiwa tu na habari yetu hakuna kitakachoendelea, ni mbaya kuliko ubaya wenyewe. Sasa tuna jambo moja tu la kufanya, nalo ni kuhakikisha hukohuko aliko sijuini Muhimbili afie huko,” Mikhail akawaambia wageni wake. “Kumkosa tumefanya bonge la mistake…” akamalizia. Laiti ungemsikia wakati anaongea Kiswahili ungedhani ya kuwa ni Mzaramo. Lakini Mikhail Planchkov alikuwa jasusi la kutisha lililotumikia idara ya ujasusi ya SVR kwa miaka kadhaa. Na sasa alikuwa kwenye moja ya kazi za siri nchini Tanzania.

“Tunatakiwa twende na muda ili mipango ikae sawa. Suala la juzi kabla hawajapata majibu, sisi tuwe tayari nje ya Tanzania na mzigo. Fanyeni kazi mlipwe pesa lakini hakikisheni msiache nyayo nyuma! Kila kitu nimeshakufundisheni,” Mikhail akawaambia vijana wake. Ilionekana wazi hakufurahishwa na kuikosa roho ya Madam S siku mbili nyuma. Mikhail alikuwa katika mpango mchafu wa kuhakikisha mfumo wa kuendesha na kulinda vinu vya nyuklia kule Bahi na Namtumbo unaibwa. Ni kifaa hicho chenye ukubwa wa tofali na uzito usiotegemewa kilikuwa na uwezo wa kufyatua makombora machache yaliyotengenezwa na wanasayansi wa Kirusi katika moja ya vinu hivyo. Tanzania ilikuwa imepiga hatua katika urutubishaji wa urani pekee katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara. “Kwahiyo, mtu yuleyule hakikisheni mnammaliza ndani ya saa ishirini na nne, asanteni,” alimaliza mazungumzo yake na kuachana na wale vijana. Mikhail aliingia kwenye ofisi yake nyingine na kujitupa kitini, akashusha pumzi ndefu na kuisogeza kompyuta yake ndogo iliyokuwa mezani hapo. Akaandika kumbukumbu fulani, na alipojiridhisha kuwa taarifa hiyo ipo sawa akafunga ile kompyuta na kuitia kwenye mkoba wake. Akaitazama saa yake, ilikuwa imetimu saa kumi jioni. Alainua simu yake iliyokuwa mezani na kubofya namba fulani alizozihitaji. Akaiweka sikioni.

“Nipe ripoti,” akasema.

*“Mzigo tayari upo kwenye boti, kila ulichotuelekeza tumefanya sawasawa, safari ya kuelekea Madagaska kupitia Comoro itaanza muda si mrefu,”* sauti ya upandde wa pili ikamwambia.

“Vizuri sana, na vipi kuhusu usalama watu wetu wanasemaje? Maana tunapousafirisha huo mzigo lazima tujue na

tulipoutoa papoje… kama nilivyokwambia, kila anayejua jambo hili na aliyehusika kwa namna moja au nyingine, anapaswa kufutiliwa mbali," Mikhail akamwambia mtu huyo anayeongea naye.

*"Kwa upande wa usalama pale Dar es salaam mpaka sasa nimehakikishiwa hali ni shwari kabisa, watu wetu wanasema hakuna hata swali waliloulizwa iwe na polisi au jeshi,"* akajibu.

"Jamson hilo siyo la kujivunia… mbwa mbaya ni yule hasiyebweka maana hujui makali yake, sasa hakikisha mzigo unafika Antananarivo salama. Nami nitaungana nayi pale baada ya siku saba, naangalia kwanza huku mambo yanaendaje. Pale Antananarivo mtapokelewa na Colonel Marvik, maelekezo yote anayo yeye," Mikhail akatoa maelekezo.

*"Na huyu mwanamke tumfanyeje? Maana nay eye kazi yake keshamaliza hawezi kuwa sumu kwetu endapo tutamwacha huru?"* Jamson akauliza.

"Aaaaan huyo hakikisha anafika Antananarivo, mkabidhi kwa Marvik yeye anajua nini cha kufanya, uwe na safari njema! Hakikisheni usalama wa hiyo Kokwa," Mikhail akatoa maagizo.

✠ ✠ ✠

Katika maji makubwa ya Bahari ya Indi, meli kubwa ya mafuta iliyong'oa nanga katika Bandari ya Mtwara kuelekea Afrika Kusini ilishusha nanga na kuegesha mahala hapo. Ndani ya meli hiyo mlikuwa na wafanyakazi kumi na watu wengine watano. Katika hawa watu watano, kulikuwa na wanaume wanne na mwanamke mmoja. Mwanamke huyu aliyekuwa hana fahamu alilala tu katika kitanda kidogo bila kujua lolote linaloaendelea. Pamoja naye walikuwapo wanaume hao wanne,

wote wanajeshi wa Kirusi waliokuwa Tanzania kwa kazi maalum. Na kazi yao kubwa ilikuwa kuhakikisha Kokwa inapatikana na inaibwa kwa uslama zaidi.

Wakiwa katika chumba hicho, simu ya ukutani iliita, alikuwa Jason aliyeinyakuwa na kuiweka sikioni. *"Jiandaeni kwa safari, naona boti yenu inawasili nusu saa ijayo,"* ulikuwa ujumbe uliyotoka kwenye ile simu kutoka kwa nahodha wa ile meli kubwa. Jason akaipachika ile simu mahala pake na kuwageukia wenzake.

"Tunaondoka, jiandaeni…" akawaambia. Basi, kila mmoja akainuka na kuchukua vifaa vyake. Jason aliweka vizuri ile Kokwa kwenye mkoba wake na kuuvaa mgongoni. "Hakikisheni huyo mwanamke yupo salama, mvikeni boya la usalama mumbebe," Jason akawaambia. Kisha akampa ishara mwanaume wa kwanza kuto kisha akafuata yeye, akafuata mwingine aliyemuweka yule mwanamke mabegani pake na kisha akamalizia mwingine. Wakazipanda ngazi mpaka ghorofa ya pili kisha wakatoka nje ya ile sehemu ya mabaharia. Jason aliiona kwa macho yake boti iliyokuwa ikiwasili hapo taratibu. Akawashukuru wale manahodha na mabaharia. Kupitia ngazi ndefu ya kamba ngumu iliyoteremshwa kutoka melini mle, wale jamaa waliteretmka mpaka kwenye deki ya ile boti na kupokelewa na nahodha wa kike aliyewakaribisha kwa heshima. Wote walipoingia ndani ya boti ile, yule mwanamke nahodha akaanza safari hiyo ya kuelekea Madagaska.

Katikati ya safari, mwanamke yule alizinduka kutoka katika mzimio aliokuwa nao. Akaanza kuweweseka na kupiga kelele zilizomshtua kila aliyekuwa amelala. Jason alikuwa wa kwanza kufika pahala pale na kumdhibiti.

“Tulia, tulia tulia,” akamwambia kwa sauti ya upole.

“Niko wapi? Niko wapiiiiii? Na we ni nani?” yule mwanamke akauliza kwa kelele. Akili yake bado haikuwa sawa.

“Hapa tupo katikati ya bahari,” Jason akamjibu.

“Bahari? Baharini tunafanya nini… Kokwa iko wapi? Mmeiba kitu kikubwa sana katika nchi yangu ya Tanzania. Najuta kutumiwa nanyi… tanzania itawaadhibu hamtofika mbali,” yule mwanamke alizidi kubwabwaja. Jason akawatazama wenziwe ambao walikuwa wamefika hapo, kisha wote wakacheka. Cheko lililoonesha dharau ya wazi.

“Chekeni tu, ila ipo siku mtalia,” akawaambia.

“Unaitwa nani kwanza?” Jason akamtupia swali.

“Naitwa Afrika!” akajibu. Mwanamke huyu wa kadiri ya miaka ishirini na tisa hadi thelahini nan ne hivi alikuwa amesahau hata jina lake. Kilichokuja kichwani ndicho alichojitambulisha. Afrika!

“Afrika?” mmoja wa wale wanajeshi akauliza kupata uhakika.

“Ndiyo naitwa Afrika, ninyi mliniiba…” akaendelea kuzungumza. Wale jamaa wakaongea kwa lugha yao ya Kirusia na kisha wakamdunga sindano ya usingizi. Afrika akapitiwa na usingdizi mzito. Ule wa kwanza ulikuwa wa kuzimia na huu wa sasa ulikuwa wa dawa. Lile boti likaendelea kukata maji usiku kwa usiku.

“Saa moja ijayo tutakuwa Madagaska… hivo mwapaswa kujiandaa,” yule nahodha mwanamke akawapa taarifa Jason na wenzake. Saa kumi na moja alfajiri, waliwasiri katika bandari bubu ya Maintirano, Maghalibi mwa kisiwa hicho kikubwa cha Madagaska. Wakateremka na kupokelewa na watu wengine

wawili ambao hawakuwatambua kwa sura zao. Mmoja alikuwa mtu mzima sana kiasi kwamba hata ngozi yake ya uso ilikwishaanza kuwa na makunyanzi na mwingine alikuwa kijana aliyevaa kama askari binafsi, nguo nyeusi na mikono yake ilifunikwa kwa glavu nyeusi. Pembeni yao kulikuwa na gari kubwa la kisasa, Toyota Land Cruiser. Hili lilikuwa ni moja ya magari hadimu kuonekana katika Madagaska. Wale wanajeshi na mzigo wao na yule mwanamke aliyejitambulisha kwa jina la Afrika akiwa bado katika usingizi mzito walipanda kwenye lile gari pamoja na wenyeji wao. Safari kuelekea pasipojulikana ikaanza.

✠ ✠ ✠

Jipatie riwaya mbalimbali za kijasusi. Tuandikie Whatsapp

**0766974865**